# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

…Kwa Neno Lako…

Lima, Peru
5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 2, Februari 2019

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


Mhariri



## Kutano ni Zawadi

Neno kutano lina asili na maana rahisi sana: ni mwelekeo wa mwendo ambao huondoa kivuli cha uadui dhidi ya kile kinachozuia kukutana. Kwa hiyo kawaida linamaanisha kujikuta mbele ya... kutaniko la kwanza ambapo mtu hufanya ni kukutana na maisha. Na katika maisha hugundua zawadi ya kwanza, mwanga wa yule ambaye anatembea kumwelekea yeye ili kumfanya ashiriki katika uumbaji wake. Toka mwanzo wa kuzaliwa kwake, mtu ni mhusika mkuu asiyefungwa na masharti ya kukutana kama zawadi.

Zawadi hii inamsaidia kila mwanadamu kutambua uwepo wa Muumba kwenye uso, kwenye tabasamu, kwenye kuangalia, kwenye ishara, tukio au katika uzuri wa viumbe. Katika kila tukio ndogo, katika kila vitu vidogo tofauti vinavyoonekana vya ulimwengu. Kwa sababu yote yaliyopo yametolewa kwa muujiza wa Roho wa Mungu ambaye amempa mwanadamu kile ambacho kimsingi ni zawadi kubwa zaidi na kamilifu zaidi: imani.

Kwa sisi Wakristo kukutana hutajirishwa na maana ya kina ya fumbo la Umwilisho. Kutoka wakati huo na kuendelea, Mkristo anaishi katika kutafuta uwepo wa Kristo duniani na katika historia, katika juhudi endelevu za kutano ambalo linaweza kubadilisha moyo wake.

Kwa hiyo kutano la uhakika na wengine, ambalo huweka katika mwendo mchakato wa kiroho, huleta ukuaji. Na katika mchakato huo, Mungu hujifunua mwenyewe kama uwepo ambao huomba ili kutufunulia njia ya kufuata. Yeye anatutangulia ili panapotokea mashaka tubaki imara katika uhakika wa misaada yake.

Ukaribu wa kumbatio unaoonekana katika kutano kati ya tamaduni tofauti, kati ya maoni tofauti, kati ya rangi na sauti tofauti. Kwa hiyo kutaniko linakuwa kabiliano na chombo cha upendo chenye uwezo wa kuangaza roho na kuufanya uwe tayari kupokea zawadi. Zawadi ambayo ni ishara na ambayo huweka alama. Kwa kuwa zawadi hiyo hutubadili na kutuwezesha kufanya daraja la kuvukia ili kuweza kumfika Kwake, kwa Baba, kwenye mapenzi yake, kwenye ukuu wake, kwenye uzuri wake usio na mipaka.

Sisi Waabuduo tunajisikia sehemu ya safari hii ambayo inatupeleka kwenye kutano, kwenye pambano, kwenye kupokea ili kutoa, lakini zaidi ya yote ili kuweza kuendelea kuwa macho na kuendelea kuchambua Uwepo Wake katika alama za nyakati.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- ◇ Kutano ni zawadi 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- ◇ Tamasha la nyimbo la kimashirika la Epifania: 6 Januari 2

*Toka Ulimwengu ASC*
- ◇ Toka Liberia 3
- ◇ Kijiji cha Matumaini 4
- ◇ Navodaya - Mysuru 5
- ◇ Dharura wakati wa Baridi 6
- ◇ Maandamano ya amani mbele ya kanisa la Mt Joseph huko Rankweil, Austria 7

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- ◇ Msaada wa Kisheria 8
- ◇ Kwa Neno Lako….Upendo mlangoni 9

*Ndani ya Shirika*
- ◇ Kalenda ya maadhimisho ya miaka 185 ya kuanzishwa kwa shirika 10
- ◇ Kalenda ya Uongozi Mkuu 11
- ◇ Sikukuu za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha 11
- ◇ Waliorudi Nyumbani kwa Baba 11

# Tamasha la Nyimbo la Kimashirika la Epifania: 6 Januari

Kwenye Nyumba Kuu liliandaliwa tamasha la nyimbo za kuzaliwa la kimashirikia, muda wa kusherehekea ambao umetuwezesha kuishi Noeli kwa ajili ya kile ambacho kwa uhalisi ni: mapokezi ya Mtoto Yesu ambaye anawafanya wote wana wa Baba mmoja.

Mada ya tamsha la nyimbo ya mwaka, lililofanyika mchana wa tarehe 6 Januari, ilikuwa: Epifania: Usiku wa Upendo, kufuata nyota".



Mada ambayo inaeleza kikamilifu maana ya tukio hili, ufunuo unaoonekana wa Mungu kupitia mwanga, Ujio Wake ulimwenguni, ambao umemwezesha mwanadamu kuweza kufanya na kujifanya chombo ili kujenga safari yake, akisikia kupendwa na upendo usio na mwisho wa Mtoto Yesu.

Mtoto ambaye, kwa kuzaliwa kwake, ameangazia viumbe akitoa uzima mapya kwa roho, ambao huzijaa na zaidi sana hutoa chakula kipya ambacho hulisha imani.

Binadamu mbele ya Mtoto Aliyezaliwa anajisikia mpya, aliyeangazwa na kuongozwa kutoka gizani. Roho yake, kama ile ya Wafalme Mamajusi, anaamini ile Yota ambayo inaangaza usiku ili kumwongoza katika uhakika wa kujisikia kupendwa na Bwana.

Mtoto Yesu amepanua mikono yake midogo kuuvisha ulimwengu uzuri katika uzuri wa milele wa upendo wake, ili kuangaza pia mioyo iliyo zaidi gizani, ili kubadili giza katika tumaini, lile la kuweza kukutana na Ufunuo.

Mungu amejifunua kwa wanadamu kupitia Mwanaye ambaye amejimwilisha kwa ajili ya wanadamu wote. Kila binadamu, bila shaka, anatafuta mwanga, ule ambao Yesu ameuleta duniani ili uweze kuongoza mioyo na kugundua uwepo Wake. Na Uwepo huu upo kila siku tunayoishi, katika sala na katika hamu ya kutoka nje ya giza, kwa sababu katika kusambaza mwanga anatoa pia upendo wake, upendo Wake usio na mipaka na masharti.

Hivyo mada hii ilijikita ndani ya tamasha la nyimbo katika msingi wa maneno yaliyoandikwa na kuhaririwa na Sr. Nadia Coppa, ikiwa na nyimbo za kuzaliwa zilizoimbwa na makundi mbalimbali ya mashirikia yaliyokuwepo kwenye tukio, lakini pia na kwaya ya Waabuduo iliyoongozwa na Sr. Toni Longo kwa kinanda na Sr. Marcia Kruse kwa gitaa. Moja ya nyakati za kukugusa ulikuwa ule wa kusikiliza kwaya ya watoto wa parokia ya Natività, iliyoongozwa na Bi. Lietta, lakini pia tulistaajabia dansi iliyofanywa na Jessica na Marco, wachezaji wawili wa mziki mtakatifu na wanachama wetu. Pia masista wa Tanzania na wa Benin waliimba pamoja wimbo mmoja wa kitamaduni kwa mtoto Yesu ambao ulituletea mdundo wa Kiafrika wa sherehe ya Kuzaliwa; ASC wa India walicheza dansi ya kumwabudu mtoto Yesu – Mwana wa Mungu.

Katika hali ya utulivu na iliyosikika kwa ndani, wanaparokia, marafiki wote waliokuwepo na mashirika ya kitawa waliokuja kwenye maonyesho haya walifurahi, walisali na mwishoni walitoa shukrani zao. Mwanga ulioletwa katikati ya altare, ulijidhihirisha kupitia ushiriki, upendo, na shangwe ya kushirikishana Tukio ambalo lilitoa uhai mpya kwenye ulimwengu.

Yote yalihitimishwa kwa kutakiana heri kwa upendo wa kidugu.







***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

Eneo la Bara: Africa
Mission Liberia


# Toka Liberia

...Shukrani kwa ukarimu wa wafadhili wa marekani, tunaweza kupata vitabu vya masomo kwa madarasa yote ya shule ya Mt. Patrick (vilivyotolewa na serikali, lakini vinapatikana kwenye shule za binafsi kwa malipo). Fikiri unalazimika kufundisha kusoma kwa wanafuzni 30 kwa vitabu vinne tu, hii inatokea kwa zana zingine nyingi, nimetumia muda mwingi wa likizo ya Noeli nikitoa nakala ya vitabu vya kusoma na vya hesabu, tumepata vitabu 50 kwa kila somo (hesabu, kiingereza, sayansi, fasihi na siasa kwa ajili ya madarasa ya V mpaka IX) na tumepata vitabu vya masomo kwa ajili ya madarasa kuanzia la I hadi V (vipo sita moja moja kwa kila kipindi,  kwa majuma sita). Wanafunzi watakaporudi shuleni, kutakuwa na vitabu vya kutosha kwa kila mwanafunzi, kwa kila somo. Vingine vitatengenezwa kadiri nafasi itakavyopatika ambapo tarehe 7 Januari wataanza tena masomo.

Wanafunzi hulipa dhamana ya kukodisha kitabu kwa mwaka mzima, ikiwa wanapoteza au kuharibu, wanapaswa kulipa gharama zote za kitabu, changamoto sasa ni kuwashawishi wazazi kuondokana na malipo ya dhamana. Ungozi na Kitivo wanashukuru kwa zawadi hii ya vitabu iliyofika wakati wa Krismasi na vyote tayari kwa wiki sita za kwanza za masomo, naendelea kuwaambia wasali kwa ajili ya wafadhili.

Sr. Zita aliondoka tarehe 9 Januari kwenda Schaan ambapo atabaki kwa majuma matano. Sikumpata mtu ambaye angeweza kuchukua nafasi yake kwa wiki moja au mbili, kwa hiyo nitakuwa mwenyewe. Muhula utaisha tarehe 8 Februari, na nitapaswa kuandaa mitihani na halafu kufanya tathimini kwa vipindi vya kazi, zaidi ya kufanya kazi ya kuandika orodha ya mahitaji ya kununua huko Monrovia – kwenye duka la jumla ambapo tunapata magazeti kwenye lango la kuingilia, tutaenda kule wiki ya tarehe 10 Februari, nitaenda na dreva wa askofu atakayeendesha gari.

Jambo lingine muhimu lilikuwa ni ziara ya mbunge Chie hapa Grand Cess. Mkuu wa Halmashauri, mwakilishi kwa ajili ya Liberia ni mzaliwa wa Grand Cess, watu wa hapa wanaona fahari kwa ajili yake. Baba yake mtu tajiri Bwn. Raffael Ann kama mtu mkuu; Mkuu wa Halmashauri Chie alihitimu masomo yake kwenye shule ya Mt. Patrick, alikuwa hapa siku 10, hadi Noeli, ili kutembelea vijiji vya eneo lake. Jumapili ya tatu la Majilio, aliomba Misa ya shukrani ambapo pia walikwepo mawaziri wawili wa dini ya methodist na watumishi wa serikali wa eneo mahalia. Sherehe ilikuwa ya furaha na shangwe na utambuzi kwa upande wa Mkuu wa Halmashauri Bwn Chie kwamba Mungu alikuwa wa muhimu katika maisha yake, na ilikuwa ushuhuda muhimu kwa wote waliokuwepo.



Heri kwa mwaka mpya wenye furaha nyote na shukrani kwa ajili ya barua pepe zenu na msaada wakati wa likizo na, zaidi kwa sala zenu. Tunawaomba msaada wa sala pia kwa ajili ya wafadhili wetu.

**_Sr. Therese Wetta, ASC_**



Sr Therese na Veronica



Sr Zita, Therese na Veronica

# Kijiji cha Matumaini

Baada ya ziara ya Sr. Nadia Coppa Mkuu wa Shirika, Sr. Bridget Pulickakunnel, Mshauri Mkuu na Sr. Manuela Nocco, Mhasibu Mkuu, walioifanya hapa Tanzania na kazi ya mipango ya Kijiji cha Matumaini, Region ya Tanzania inashirikisha kwa wasomaji historia na mradi wa Kijiji kupitia masimulizi ya Sr. Maria Rosaria Gargiuolo, ASC.

Kijiji cha Matumaini ni taasisi iliyoundwa mwaka 2001 na Waabudu Damu ya Kristo kupitia ndoto ya Sr. Maria Rosaria Gargiulo, ASC, mmisionari nchini Tanzania.

Sababu na madhumuni ya taasisi hii ilikuwa kujenga makazi kwa ajili watoto yatima wasiona na wazazi wote wawili, walioambukizwa VVU, hasa kutoka maeneo ya Singida, Dodoma na Morogoro, lakini inapobidi, pia kutoka mikoa mingine.

Hatimaye, tarehe 1 Januari 2002, taasisi hii ilisajiliwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii kama "Nyumba ya Watoto". Mnamo 17/8/2002, ilikuwa siku rasmi ya ufunguzi wa taasisi, baada ya kupata vibali vyote, watoto watatu wa kwanza walipokelewa. Mradi huu unapokea watoto wale tu ambao wanaletwa kwetu na Ustawi wa Jamii wanaotoka Mikoa mbalimbali.

Mradi una sehemu tatu:

***Sehemu ya kwanza:***

I) Mazingira muhimu ya Kijiji cha Matumaini kwa ajili ya kufanya utume;

- Nyumba za kuishi 12 ambazo ni makazi ya watoto yataima walioathirika na HIV/AIDS.
- Dispensari
- Maabara kwa ajili ya vipimo sahihi vya damu;
- Shule ya watoto wadogo, shule ya msingi na sekondari kwa ajili ya kufundisha watoto wenye HIV/AIDS wanaoishi Kijiji cha Matumaini na wasio wagonjwa wanaoishi kwenye maeneo jirani.
- kituo kwa ajili ya kuhudhuria wanawake wajawazito wenye HIV/AIDS wanaokuja kwa ajili kupata matibabu ya kupambana na HIV na kufundishwa kuwalinda watoto wao ambao bado hawajazaliwa na maambukizi ya HIV.
- Jengo la utawala na nyumba ya masista, ofisi ya mradi wa Kijiji cha Matumaini;
- Zizi kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa, kuku na wanyama wengine kwa ajili ya kusaidia lishe bora kwa ajili ya watoto wa Kijiji cha Matumaini.

II) Lengo la mradi toka mwanzo mwanzo lilikuwa ni kuwapokea watoto wote wenye HIV/AIDS yatima waisio na wazazi wote wawili au waliotelekezwa. Watoto yatima wanaishi katika familia na wazazi wa kambo kama "ndugu wa nyumba." Makazi yaliyopangwa yanaweza kupokea jumla ya watoto yatima 109 wanaopelewa katika familia 12, lakini kwa sababu ya mahitaji makubwa tumelazimika kupokea watoto zaidi, watoto tuliowapokea katika nyumba za familia ni 163.

Kijiji cha Matumaini kinatoa kwa hawa watoto yatima wenye HIV/AIDS mazingira ambayo yanasitawisha tunu za familia na kuwatibu kupitia tiba ya kupambana na virusi kwa dawa zinazofaa, kutoa misaada ya maabara na wauguzi, kuwapa chakula bora ili kushughulikia mahitaji yao ya lishe, ya kisaikolojia na ya kiroho ili kuwawezesha kukua na kufanikiwa licha ya changamoto zao.

***Sehemu ya pili: "Mpango wa kuwafikia walio nje"***

Sehemu ya pili ya Kijiji cha Matumaini ni upanuzi wa mpango huo hapo juu kwa ongezeko la watoto wengine 400 na familia zao wenye VVU/UKIMWI wanaoishi katika hali salama na ya kukubalika katika maeneo yaliyo karibu na Kijiji cha Matumaini au eneo la Dodoma. Watoto yatima wenye msaada toka ndugu wa familia, huhudumiwa kupitia mpango huu. Wagonjwa wanapatiwa tiba ya kupambana na virusi wakiwa wanaoishi majumbani mwao.

***Sehemu ya tatu: Uzazi salama***

Sehemu ya tatu ya mradi wa "Kijiji cha Matumaini" ina lengo la kulinda uhai wa mama mwathirika, kwa kupewa tiba ya kupambana na virusi, ili kuzuia maambukizi kwa mtoto na kuhudumia familia nzima kwa kutoa elimu wakati wote wa matibabu yake "kwenye Kijiji cha Matumaini". Wanawake wawatafuataliwa muda wote wa ujauzito na kupewa matibabu yanayofaa na elimu kama wagonjwa wa nje. Pale wanapokutwa na maambukizi ya juu wanalazwa kwenye Kijiji cha Matumaini kwa ajili ya matibau makubwa kwa wiki kadhaa kabla ya tarehe ya kujifungu iliyotarajiwa na kubaki hadi miezi mitatu baada ya kujifungua.



*Maelezo – toka Historia ya Kijiji cha Matumaini iliyotolewa na Sr. Maria Rosaria Garigiulo, ASC, wakati wa Mkutano wa Mwaka wa Region*

Eneo la Bara: Asia
Region India

# Navodaya - Mysuru

Sisi ASC tunafanya kazi katika vijiji 25 vya Karnataka kwa ajili ya maendeleo na uelimishaji wa wanawake kupitia mipango ya kujitegemea inayoitwa Sanghas. Katika mradi huu tunashirikiana na kundi la KHPT ambalo linasaidia Karnataka kwa kukuza afya na ustawi kwa familia zilizoathirika na UKIMWI au ambazo zinakuwa na matokeo chanya ya VVU. Wanapokea msaada wa kifedha kuanzisha biashara ndogo na hivyo kutiwa moyo kukabiliana na matatizo ya maisha.



Katika vijiji 7, kwa upande mwingine, tunatoa msaada wa kiuchumi kwa watoto 10 ambao wamejiunga na shule za umma ili kusaidia elimu yao. Katika kila kituo Bunge la Watoto lilianzishwa, ili kuchochea ushiriki na wajibu katika kujibu jitihada zao.

Katika vijiji ambapo tunatoa huduma kuna pia wajane wengi, ili kuwasaidia tumeandaa kundi watu 65 kati yao hushiriki kozi, ambapo wanapewa kozi za kitaaluma na kupitia mkopo tunatoa pia msaada wa kiuchumi.

Kozi za kushona na kompyuta zinatolewa kwa wasichana, wajane na watoto ambao wameacha shule, kuwaandaa kukabiliana na maisha kwa kujitegemea. Sr. Celine, mshauri wa Region, aliwapa semina ya mafunzo juu ya maendeleo ya kibinadamu, ambayo pia ilihudhuriwa na wanafunzi wa NTC na wafanyakazi wa Navadoya.

Mnamo Oktoba 2 wakati wa siku ya kuzaliwa Mathma Ghandi, wanafunzi wa NTC waliandaa maonyesho ya kazi zote za mikono ambazo walifanya kwa vitu vya mabaki. Mnamo Novemba 1, kwa ajili ya sherehe ya Kannada Rajyotsava, tuliandaa kwa ajili ya watoto wote wanaoishi na wazazi wa kambo, sikukuu pamoja na michezo, shughuli za kisanii, mashindano, majaribio ya kumbukumbu na maswali.



Tarehe 11 Novemba tumeadhimisha, pamoja na watoto 200 ambao tunawasaidia kiuchumi, katika Kituo cha Jamii cha Novadoya (watoto wa kijiji), Siku ya Watoto ya Kimataifa na Deepavali (moja ya sherehe muhimu zaidi za kihindi, huadhimishwa mnamo Oktoba au Novemba inayoonyesha ushindi wa wema dhidi ya uovu na inaitwa "sikukuu ya mianga"), tuliandaa mashindano ya nyimbo, utani na mashindano ya ngoma, tukigawa zawadi mwishoni mwa mashindano. Kisha Desemba 21 tuliadhimisha Krismasi na watoto wa vijiji wanaoshiriki katika masomo ya kurudia mitihani yanayotolewa bure, na walifurahia sana.







Tunashiriki ndoto ileile ya Mt. Maria De Mattias na kwa namna ya uhakika, kwa njia ya shughuli zetu nyingi, sisi pia tunahakikisha kwamba inatekelezwa. Ninaishukuru jumuiya yangu kwa msaada, ushirikiano na ushiriki hai wa kazi katika kila tukio. Kwa pamoja tumewafikia maskini wengi zaidi, hasa wanawake na watoto wa vijiji hivi. Tunamshukuru Bwana kwa neema zote ambazo ametupa. Tufanye upendo wake, kujali kwake na jina lake litukuzwe kupitia uwepo wetu kati ya wenye mahitaji zaidi.



***Sr. Jaicy Karukuttikaran, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

# Dharura wakati wa baridi




Tarehe 6 Desemba 2018, mbele ya Mkuu wa Region, Sr Nicla Spezzati ASC, Meya wa Latina Damiano Coletta, mkuu wa baraza la huduma za kijamii Patrizia Ciccarelli, na askofu Mariano Crociata, ilifunguliwa rasmi huduma ya dharura ya baridi na mabweni kwenye makazi ya zamani ya Shirika ya Damu Azizi ya Viale XXIV Maggio huko Latina.

Jengo litawezesha mapokezi ya watu sitini wahitaji, litabaki wazi wakati wa baridi hadi Machi, kila usiku, kuanzia saa 19. Kwenye mabweni watu wenye hali ngumu ya kijamii watapata mazingira ya joto ambapo watalala usiku, mahali pa kuoga na asubuhi wataweza kupata kifungua kinywa.

Mradi huu uliwezeshwa kwa ushirikiano wa pamoja wa "Tre Fontane" wa Kikundi cha Cascina. Manispaa ya Latina imewakabidhi wao huduma hiyo kupitia zabuni ya umma. Kitashirikiana na makao makuu ya mji na masista waliotayari kujitoa kwa ajili ya mapokezi na kwa tabasamu.

Siku ambayo uzinduzi mkuu ulifanyika, kulikuwa na hisia ya mguso kwa washiriki wote kuona mradi ukitimizwa ambao una ladha yote ya "Kanisa linalotoka", kwa sababu linahusisha Watawa Waabuduo Damu ya Kristo, ambao wamejiunga kwa shauku kubwa na taasisi za siasa, wanatoa jibu kwa umasikini wa leo. Haya maneno ya raia wa kwanza: "Katika siku za hivi karibuni tumezungumzia haki za binadamu, leo tunafanya kitu halisi kwa kuanzisha muundo wa kukaribisha walio maskini".

Ni furaha kubwa zaidi kati ya masista ambao wanaona katika uanzishwaji huu nafasi kubwa ya kusali kwa ajili ya yule anayeingia na anayetoka kwenye taasisi na kumsindikiza kwa kujali mwendo wa wasiwasi na mahangaiko ya hawa ndugu zetu wasio na kitu.





***Sr. Emma Zordan, ASC***

# Maandamano ya amani mbele ya kanisa la Mt. Joseph huko Rankweil, Austria

Tarehe 25 Novemba 2018, nje ya kanisa la Mt. Joseph huko Rankweil, Austria yalifanyika maandamano ya amani kwa ajili ya kuwakumbusha wakristo wajibu wa kuwatunza wakimbizi na wahamiaji. Padre aliyeandaa tukio hili, Pd. Wilfried Blum, rafiki wa ASC wa Region ya Schaan, alitaja katika mahubiri yake sanaa ya madirisha ya kioo, yaliofanywa na Jutz Waldner yenye kingo ndefu, ambayo yanatoa mkazo wa maandiko matakatifu kwa hili hitaji la ulimwengu wa sasa. Moja ya madirisha limechorwa picha ya familia takatifu inayokimbia kwenda Misri ili kumwokoa Mtoto aliyekuwa anatafutwa na Herrode (Mt. 2:13-15). Familia Takatifu ililazimika kukimbia kwenda nchi ya mbali ya kigeni, na wenyewe walipata kuwa wakimbizi, kama hawa wa sasa.



Padre Blum pia alibainisha kuwa Biblia imejaa habari za watu wanaokimbia na jinsi Mungu anavyowasaidia. Kitabu cha Kutoka (22,21), kinatoa maelekezo wazi kwa "watu wenye mapenzi mema" kuhusu mgeni: " Usimtendee vibaya au kumnyanyasa mgeni, kwa sababu wewe ulikuwa mgeni katika nchi ya Misri". Kitabu cha Mambo ya Walawi (19: 33-34) kinasema: "mgeni anapokaa kati yenu katika nchi yenu, msimtendee vibaya, mgeni anayekaa kati yenu anapaswa kutendewa kama mmoja wenu. Mpende kama ujipendavyo, kwa kuwa wewe ulikuwa mgeni huko Misri. Mimi ni Bwana Mungu wako. Hatupaswi kusahau maneno ya Yesu kuhusu hukumu ya mwisho, vigezo ambavyo tutahukumiwa, matendo ya huruma: "Nilikuwa mgeni ukanikaribisha ..." Mt. 25:35).

Wajibu wetu kama "watu wenye mapenzi mema", kama wakristo, Blum amesema, sio wa kufunga macho mbele ya wajibu wetu kuhusu wahamiaji na wakimbizi, bali tunaitwa kuwapokea na kujiunga nao katika kutafuta kwao uhuru na maisha bora. Zaidi ya hayo tutakuwa tunasaliti chimbuko letu la kiyahudu-kikristo.

*Sr. Maria Hammerer, ASC*

# Msaada wa kisheria

## Kuwa sauti ya wale wasio na sauti



Nilipokuwa mnovisi niliona makala nzuri iliyoandikwa na sista mmoja, mwanasheria mshuhuri ambaye alisaidia watu wasioweza kujitetea, hasa wale ambao hawakuwa na uwezo wa kufikia mlango wa mahakama kwa sababu hawakuwa na pesa za kumlipa mwanasheria na kupigania haki. Niliguswa sana na wanawake hawa mashuhuri ambao wamekuwa na shauku kubwa na bidii ya kufanya kazi kwa ajili ya wale waliogandamizwa ambao bado wapo hata leo, ni wao hasa ambao leo wananihamasisha kuwasaidia wahitaji, hasa wale ambao wananyimwa uhuru wa kihisia, kimwili na kisaikolojia.

Mbegu hii ilimea na kukua ndani mwangu ikinihimiza kufanya kazi hii ili kuwa sauti ya wale walio wa mwisho katika jamii.

Nilifanya bidii katika masomo ili kupata shahada ya sheria. Leo ninahusika hasa na masuala yanayohusiana na wanawake, unyanyasaji wa majumbani, ukatili, shida za kifamilia na kupambana kwa ajili ya haki zao na kesi zinazohusu haki zao za mali za urithi. Kama mwanasheria mtawa, mimi pia ninajitolea kusaidia watu nikitafuta nafasi kwa ajili ya watoto wanaoteseka katika familia kwa sababu ya wazazi kutengana. Wateja wangu wananiamini hata zaidi kwa sababu mimi ni mtawa.

Pia ninaongoza mipango ya kusoma sheria katika maeneo mbalimbali kama vituo vya kijamii, kuwaelimisha wanawake, wajane na watoto kuhusu haki zao. Ninawafundisha jinsi ya kuwasilisha FIR (First Information Riport and registration of case/Ripoti ya Kwanza ya Habari na kuandikisha kesi) kwa kufuata mchakato mzima. Nilipata pia fursa ya kuongoza semina kwa wanawake juu ya "unyanyasaji wa kijinsia mahali pa kazi".

Kuwa sista mwanasheria inanipa fursa ya kupanua huduma yangu kwa watu maskini, wahitaji na wanaogandamizwa. Mimi pia natambua fursa na msaada ambao shirika na jumuiya limenipa kwa kuniandaa ili kuleta mafanikio katika huduma hii.

Mtakatifu Maria De Mattias, Mwanzilishi wetu aliyefanya kazi kwa maskini na wanawake ni msukumo na mfano wa kurejea kwa ajili ya kufanya kazi yangu kama mwanamke aliyewekwa wakfu.

Wakati umefika kwa wanawake kutetea haki zao za kijamii, kupinga ndoa za utotoni, mfumo wa mahari, unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji wa majumbani.

Nikiangalia nyuma, ninamshukuru Mungu kwa kunipa fursa ya kufanya kitu tofauti: kuwa sauti ya wale wasio na sauti.



***Sr. Shiny Kayyaniyil, ASC - Advocate***

# Kwa Neno Lako....Upendo Mlangoni



Sisi Waabuduo tunakumbatia mchakato wa Mabadiliko na tukifanywa wapya kwa moto wa Karama yetu, tunatangaza Nguvu ya Damu ya Kristo kwa wote tunaokutana nao Hati za MK 2017). Mnamo Januari mwaka jana, pamoja na Sr Nadia, nilipata fursa ya kutembelea Parokia ya Kuzaliwa Mama Yetu ambapo wanahudumia wahitaji na wenye njaa. Katika kuangalia hali halisi ya watu waliopo, macho yangu yalifunguliwa, moyo wangu ukaguswa na nilishangaa kuona watu hao wote wakiwa kwenye mstari wakisubiri kupokea chakula. katika kuzungumza na baadhi yao niligundua kwamba walikuwa wakimbizi na wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Wengi wao hawana nyumba, chakula na kazi. Baadhi yao wamepoteza mali zao na wapendwa wao, wengine wamekimbia kutoka nchi zao kwa sababu ya vita na majanga ya asili, au walikosa mwelekeo kwa sababu ya mateso na maumivu waliyoteseka n.k ...

Nilijiuliza: kwa nini nilichagua maisha ya wakfu? Je! Ni kwa ajili ya usalama wangu au kwa ajili ya upendo kwa Mungu na kwa watu wake? Mageuzi yalitokea moyoni mwangu ambayo yaliniwezesha nitoke nje ya mlango wangu. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, nilijipa moyo ili kukabiliana na changamoto. Changamoto zangu zilionekana katika ugumu wa mawasiliano, utofauti wa tamaduni, watu, chakula. Lakini kila Jumatatu na Alhamisi alasiri nilihisi kuwa na nguvu tele na shauku ambazo zinanisukuma kwenda parokiani. Nilishangazwa na roho na bidii ya watu wanaojitolea ambao hutumikia watu hawa wote wenye njaa ambao husubiri mlangoni kwetu. Mara kadhaa, nimeweza kujifunza kutoka kwao tunu za Ufalme kama .. Upendo, Haki, heshima kwa kila mtu, mahangaiko kwa ajili ya wadhaifu na wanaotengwa, kushirikishana, mshikamano, msamaha, amani, nk ... Nakumbuka mtu aitwaye Danieli ambaye siku moja, alilewa, alipiga kelele kwa wengine, akisema maneno mabaya kwa lugha zote na kufanya vibaya, nk. Katika hali hiyo, bila kujua nini cha kufanya, niliona hali ya mtazamo wa watu wanaojitolea. Kwa mshangao wangu mkubwa, niligundua kwamba wote waliendelea kubaki wema, utulivu, mwenye huruma na walijaribu kusikiliza na kuelewa kile alichotaka. Wakati huo maneno ya Injili ya Mtakatifu Mathayo 25, 35-36 yalirudi kwenye akili na moyo wangu "Kwa kuwa nalikuwa na njaa mkanipa chakula, nalikuwa na kiu mkaninywesha, nalikuwa mgeni mkanikaribisha, nalikuwa uchi mkanivika, nalikuwa mgonjwa mkanitunza, nakuwa kifungoni mkaja kunitazama".

Haya ni maneno ya Yesu yaliyonihamasisha kumtumikia na kufanya mang'amuzi ya kuongezeka mikate na samaki, juu ya mlima pamoja na Yesu. Mamia ya watu walikula na kushiba na mabaki mengi yalibaki. Kila mara mezani wanakuja kula watu 400 – 500 na chakula kinachotolewa kila mara kinatosha. Muujiza huu unatendeka shukrani kwa utayari na ukarimu wa mioyo na mikono mingi.

"Chochote unachomtendea mmoja wa hawa ndugu zako walio wadogo, umenitendea mimi". Namshukuru Bwana kwa sababu mimi ni wa thamani machoni pake kwa kunijalia baraka tele.





***Sr. Rani Padayattil, ASC***

# Kushirikiana na kristo katika kazi ya ukombozi.

## Kalenda ya maadhimisho ya miaka 185 ya kuanzishwa kwa shirika
## 2019 – 2020

- 1-4 machi 2019 – **Kamati Kuu**
- 4 april 2019 – **CIS**
- 4 mei 2019 – **Brazil**
- 4 juni 2019 – **India**
- 4 julai 2019 – **Argentina, Bolivia na Spagna**
- 4 agosti 2019 – **Polonia**
- 4 septemba 2019 –**Schaan**
- 4 oktoba 2019 – **Tanzania**
- 4 novemba 2019 – **Stati Uniti**
- 4 disemba 2019 – **Zagreb**
- 4 january 2020 – **Corea na Filippine**
- 4 february 2020 – **Italia na Guinea Bissau**
- 4 machi 2020 – **CIS**



# Kalenda ya Uongozi Mkuu




**1-3 Februari –** Adhimisho la sala ya siku Tatu kwa ajili ya Sikukuu ya Mt. Maria De Mattias
**4 Februari –** Adhimisho la Sikukuu ya Mt. Maria De Mattias
**23 – 24 Februari –** Mkutano USMI: mada "familia na shule kwa ajili ya elimu na usindikizaji wa vijana" atashiriki Sr. Nadia Coppa

## Sherehe za kuzaliwa: tunasherehekea maisha

| | | |
|---|---|---|
| miaka 30 | | |
| **Sr. Sarah Harbaugh** | 23/02/1989 | USA |
| miaka 60 | | |
| **Sr. Lucja Lis** | 07/02/1959 | Wrocław |
| miaka 70º | | |
| **Sr. Giuseppina Debiase** | 26/02/1949 | Italia |
| **Sr. Anna Maria Vissani** | 13/02/1949 | Italia |
| **Sr. Paula Antolović** | 25/02/1949 | Zagreb |
| **Sr. Kochuthresia Akkunnath** | 20/02/1949 | India |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Filomena D'Andrea** | 07/02/1939 | Italia |
| **Sr. Mathild Frick** | 14/02/1939 | Schaan |





## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 06/01/2019 | **Sr. Mary Matthew Janciar** | USA |
| 06/01/2019 | **Sr. Mary John Goles** | USA |
| 06/01/2019 | **Sr. Dominika Lanz** | Schaan |
| 09/01/2019 | **Sr. Assuntina Colantoni** | Italia |
| 12/01/2019 | **Sr. Ann Connolly** | USA |
| 14/01/2019 | **Sr. Helen Panci** | USA |
| 29/01/2019 | **Sr. Geltrude Valletta** | Italia |

**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 2, Februari 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*